Kama unataka kupata msaada ya mafasiriyo toka kwa mumoya wetu njo kisha ujiandikishe kukuwa mumoja wa Kundi ya Wanamemba wa Survivor Alliance, tafazali  ututumiye barua pepe (email) kuhusu mambo yenye inaandikiwa hapa chini mu luga ya Kiingereza. Hii itatusaidia kufahamu kama itakuya hitajika kupata mtu wa kusaidia kuhusu tafsiri ya lugha wakati ya kuzungumza na weye.

Inahusu : *Interested in joining Survivor Alliance*

Ujumbe:

*Hi, my name is* [andika jina] *and I want to speak with someone about the Survivor Alliance. I speak* [andika luga yenye unasemaka] *language.*

*I am able to speak the following dates and times:*

[weka tarehe na saa gani unaweza kutapata wakati ya kuzungumuza. Tujulishe njia tatu za uwezekano kuhusu saa gani na gani. Tafazali tujulishe ikiwa unapatika kwenye eneo gani la wakati na kumbuka kuwa sisi tuko kwenye wakati ya UK - Uingereza]

-----

## KAZI

Kuunganisha na kuwatia nguvu waliopona kutoka hali za Utumwa na Biashara ya Wanadamu wenye kuwa kwenye inchi mbali mbali ulimwenguni kote.

## SISI NI WANANI NA KAZI GANI TUNAYANYAKA ?

- Shirika la Walionusurika ni Muungano Usio wa Kiserikali (NGO) ambayo inaunganisha na kuwatia nguvu waliopata bahati ya kupona kutoka utumwa na biashara ya wanadamu wanao geuza wengine kuwa kama bihashara dunia nzima.

- Tunafanya njia kusudi Watu ambao Waliweza Kupona toka hali za Utumwa na Bihashara ya Binadamu kugeuza wengine kuwa kama bihashara yao na ambao tayari walishaka anza kazi ya kupiganisha mabaya hii, waungane kuwa Kundi la dunia nzima.

- Tutasaidia maendeleo ya makundi ya watu walioponyoka mabaya hii, na tutaunganisha makundi yenye ilisha kuwa, hata kama iwe : kwenye miji mikubwa, kwenye majimbo na kwenye inchi mbalimbali.

- Tunashirikiana pamoja na washirika wengine katika kazi kusudi ya kuhakikisha kuwa sauti za Walioponyoka zinapewa nafasi ya mbele katikati juhudi zozote za kupambana na hali za Utumwa. Tutasaidia kutia nguvu na kuwezesha ushiriki wa Walioponyoka inapowezekana.

- Kujiandikisha katika hii Ushirika Inafanyika bila malipo yoyote, na pia mtu yeyote anaye jitambua na kujitambulisha kama mtu aliyeponyoka vidonda vya Utumwa au Biashara ya Wanadamu, na ambaye anakaa katika nchi yoyote ile, anawzeza kuomba kujiandikisha.

## KUWA MWANAMEMBA

### Inamaanisha nini kujiunga na UShirika ya Walionusurika kama Mwanamemba ?

### Itakuwezesha :

- Kuwa mumoja kati ya Ushirika wa Dunia nzima, tena wa Waliopata mafundisho mbalimbali wa Jamaa ya Watu ambao Walipata bahati ya Kuponyoka toka Tabi aya Watu Kufanya wenzao Wanadamu kuwa kama Biashara ao Watumwa.

- Kuweza kupokea, ukitaka, mashauri kuhusu jinsi ya kuandika ao kueleza habari inayo husu maisha yako / ao inayo eleza kuhusu historia ya kujulisha wengine kuhusu elimu yako na kuhusu kazi zenye ulishaka zifanya mu maisha yako.

- Kuweza kukuwa nazungumuza kwenye mutandao wa internet na Wengine ambao Wanaongoza katika kupiganisha tabia za Utumwa na kupata mashahuri

- Kuweza, wakati unaitaka, kuwa nafikiwa na jarida yetu yenye inafika kwa njia ya barua pepe (email) na ambalo tunatumikisha kusudi ya kujulisha ma occasions inayokuwa ya kuhitaji shahuri yako ao uongozi yako.
- Kuhuzuria wakati unayo taka, ku vikao yenye inakusanyaka Walioponyonka vidonda wao kwa wao tu.
- Kuleta muchango yako ya mawazo kusudi ya kufanya bora zaidi Sheria yetu ya kuhusu gisi ya kuwa Mwanamemba (Manifesto) na kutusaidia kutia nguvu jamaa hii ya Dunia nzima inayo unganisha Benye Baliponaka Vidonda mbali-mbali ya Utumwa wa Binadamu.

## Tangazo Kuhusu Hali ya Kuwa Muanamemba

Tafazali usome kila moja ya hizi habari hapa kwa makini. Tunawaomba wanamemba wote wanaotaka kujiunga nasisi kukubaliana na tangazo hizi kama mambo tunayo yakazia sana kama mambo ya kuheshimiwa.

### Tunaamini Kwamba Habari ya Utumwa na Biashara ya Wanadamu inaingiliana na Aina Nyingi za Kunyanyasana.

Kunyanyasana inaweza kutokana na jinsi hali ya maisha ilivyo kati ya makabila mbali-mbali, hali kati ya maisha ya Wanawake na Wanaume, hali kati ya kiwango cha mapato, hali kati ya Makundi ya kijamii, hali kati ya dini na dini, hali kati ya mahusiano ya kimwili, hali kati ya utaifa na taifa, hali kati ya uwezo wa mwili na kiakili za mtu, na mengine mengi.Tunafahamu kwamba mupaka leo hii, matokeo ya ile hali iliyo tokea zamani ambako watu walifanywa kuwa mateka kisheria na ile hali ya utumwa walio pitia wa Afrika bado matokeo ya hayo yanaonekana hata leo. Tunaamini kuwa ni jambo la maana kushugulikia matokeo hiyo, pamoja na kushugulikia ubaguzi mukubwa, kuimwa haki, na pia ubaguzi wa rangi wanaopitia wamoja kati ya watu weusi.

Tunaamini kwamba ni lazima kwamba kupambana na utumwa na kupambana na kule kuwafanya wanadamu kuwa bihashara viwe ni pambano la kuzuiya watu kugandamiziwa.

Lazima tuunge mkono kundi la #BlackLivesMatter, na kuunga mkono Makundi inayo piganisha kunyanyasiwa ya wanawake, na pia Makundi inayo pambana kwa ajili ya Droits (ao haki) za Wafanyakazi, haki ya watu kuchunga mazingira ya hali ya hewa ibaki safi, haki kwa kizazi cha wa Windrush, haki kwa jamii ya Kundi la LGBTQ, haki

za watu wa kiasili (Autochtones) na haki za Wahamiaji / Wakimbizi, haki za Makundi ya watu ambao bado hakuna taarifa zilizo andikwa kuwahusu, haki za Walemavu, na mambo kama na hayo.

**Tunajenga Imani yetu katika Mazungumuzo ya Kila Mtu na Mwengine, wala sio Kuzungumuza Kwa Niaba ya Kila mmoja.**
Sisi sio "sauti ya wasio na sauti". Kila mmoja wetu ana sauti yake. Kuna Wamoja wetu ambao wanajielezaka kwa njia ya Kuongea na Makundi ya watu, Kuna wengine ambao wanaongeaka kwa njia ya Kuandika, Wengine wanaongeaka kwa njia ya kufanya makazi katika jamii, kuna wengine wanongeaka njia za kutunga vitu sawa nyimbo ao kupiga picha. Tunazungumza tokana na bitu tulishaka pita amo na tunasaidiana kutiana nguvu kusudi sauti ya kila mumoja wetu isikilike.

**Tunatambua kuwa mambo tulioyapitia ndani ni ya pekee na tena yanatofautiana selon mtu na mwengine**
*Tunatambua kuwa mafasiriyo yenye Umoja wa Mataifa inapanaka kuhusu kosa la hali ya Binadamu kugeuza wengine kuwa bihashara nimafasiriyo yenye upana na inaonekana kuwa byenye kila aliye ponyoka alipitiaka amo habita jikuta kusema binafananana ku kila neno na ile mafasiriyo yenye Umoja ya Mataifa inaelezeka kuhusu Banadamu kugeuza Bengine kuwa bihasahra. Ile njo sababu, tunajitahidi kuwa na umoja kusudi ya kueleweshana na kuenezeana elimu kwa kila mumoja juu ya utofauti katika mambo yenye tulisha wahi kupitia amo na kuweza kuunganisha kila occasions inayo weza kuonekana na inayo husu mumoja kati ya benye baliponyokaka hali hizo.*

**Tunaamini kuwa nguvu ya neno "sisi" ni kubwa kuliko nguvu ya neno "mimi".**

*Kwa gisi Kundi la walioponyoka ni kubwa na tena watu wenye kuwa ndani wako na ma tofauti za aina mbali-mbali, inawezekana kwamba si kila wakati njo tutakuwa na maoni inayo fanana. Hata hivyo, wakati tunapokubaliana, sauti ya pamoja ituruhusu kuweka pressions (shinikizo) ku benye banatungaka sheria (viongozi), na kuweza kusimama pamoja ili kupambana na hali ya kuimwa haki, nakusimama pia pamoja katika kukusanya vifaa pamoja, na kusimama pamoja katika mambo mengi zaidi.*

**Tutatanguliza mbele afya yetu na kufanikiwa kwetu kwanza.**
*Tunatambua kuwa ni jambo la lazima kuongoza kwa njia ya kuonyesha mfano. Kusudi ya kuwa viongozi wenye kufaulu (kufikia malengo)i, wateteajii, washauri, na wanamemba wa jamii, tutatanguliza mbele afya yetu na kustawi yetu kwanza.*

**Tutakomalisha uza mawazo kuhusu Tufanye Nini Kabisa kusudi ya kutokupuuzia Kushugulikia Shida Zenye Zinatokanaka na Vidonda vya Ndani ya Mioyo (kiwewe).**
*Tunatambua kuwa vitu vinavyo tokea mu maisha na byenye binaachaka vidonda yamu moyo biko binatokea kila fasi mu dunia. Ndio sababu, tumefikia kugundua kuwa mtu yeyote, sio tu benye baliweza kuponyoka hali za Binadamu Kufanya Bengine Kuwa Sawa Bihashara, hata na bengine benye habakupita mwa ile banaweza kuumizwa na kubeba vidonda vya moyoni na tena bidonda yenye kukawia. Ndiyo sababu,tutakomalisha hali ya kutokupuuzia vidonda vya moyoni katika kila mahusiano (mazungumuzo), na hasa katika tukio ao jambo lolote*

*linalohusiana na mtu aliyeponyoka kutoka Hali ya Mwanadamu Kutendea Mwengine Sawa ni Bihashara Yake.*

**Tutakomalisha Umoja na Kujikinga na Hatari ya Magawanyiko.**

*Kwa gisi Kundi la walioponyoka ni kubwa na tena watu wenye kuwa ndani wako na ma tofauti za aina mbali-mbali,tunaaelewa kuwa hali za kuwa za watu na mitazamoya watu inaweza kufikia kutokupatana. Zaidi ya yote, tutapata msingi unao tuunganisha katika kuelekea kushugulikia hali ya unyanyasaji tulio wahi kuupitia zamani na katika kulenga kwetu pamoja kuzuia hali ya Wanadamu Kuwafanya Wengine Kuwa Kama Biashara yao, kuwalinda walioponyokaa, na katika kuwatia nguvu wae walio wahi kuponyoka hayo. Tunatarajia kila mtu kukomalisha umoja na kujiepusha na mgawanyiko.*

**Tunajitolea Kufanya Kazi Kwa Heshima Hata Katika Kupitia Changamoto na Migogoro Ikitokea.**

*Tunaamini kuwa tofauti za mawazo ni jambo yenye inatokeaka tu kwa kawaida na inaletaka pia kufaidika na mawazo ya wengine. Walakini, changamoto na migogoro ikitokea, tutajibu kwa kutumia utaratibu na tutatafuta kuyatatua kwa njia ya*

*kiraia na yenye heshima. Hatutaendeleza tabia ya "kupiga kelele". Kunapo tokea kutokukubaliana, tunawahimiza walio wahi Kuponyoka kuzungumza wao kwa wao na ana kwa ana. Ikiwa mzozo hauwezi kutatuliwa, tunatarajia pande zote kuendelea kuishi kwa njia ya utaratibu na kuchukuliana.*

**Tunatambua kuwa kila mtu ana Devoir (jukumu) ya lazima katika Umoja wa Kupambana na Hali ya Wanadamu kugeuza Wangine Watumwa na Kupambana na Mitandao inayo Wafanya Wanadamu kuwa kama Bihashara yao.**

*Tunaamini kuwa, ikiwa wanataka, walioponyoka wote wanaweza kuchukua jukumu katika Umoja wa kupambana na utumwa na kupambana na tabia ya bihashara ya wanadamu. Hakuna mashurti yoyote inayo hitajika ili kufanya hivyo na wala hakuhitajiki kwamba ifanyike hazarani. Kila aliyeponyoka iko mu safari ya kipekee na lazima aamue mwenyewe jinsi, au ikiwa, anataka kufanya hivyo.*

## Inayo Hitajika Kwa Mwanamemba

✔ Mimi najitambua kuwa mtu aliyepata kuponyoka toka hali ya Mwanadamu Kumukamata Mwanadamu Mwangine sawa Bihashara na / ao sawa Mutumwa wake.

> ***Tovuti*** :
> [https://www.unodc.org/unodc/en/human-trafficker/what-is-human-trafficker.html?ref=menuside]
>
> Mwanadamu Kumukamata Mwanadamu kuwa Kama Bihashara Yake = "Kumufanya mtu kuwa kama bihashara" inamaanisha kutia mtu mu kazi, ao kumusafirisha, ao kumuhamisha, ao kumubeba ao kupokea watu, kwa njia ya vitisho au matumizi ya nguvu au aina zingine za kulazimisha, kwa kutekwa nyara, ao kwa udanganyifu, ao kwa magendo, ao kwa matumizi mabaya ya madaraka au kwa matumizi mabaya ya hali ya unyonge au tena kwa kutoa au kupokea malipo au faida za kufikia kukubalisha utashi wa mtu anayekuwa na mamulaka juu ya mtu mwengine kwa kusudi ya kumuonea (kumunyonya nguvu, ao mali ao heshima yake).
>
> Kunyonyana nguvu, heshima, mali na kazalika inaweza kuwa pia kiwango cha chini kama unyonyaji kwa njia ya kufaidia ukahaba wa mtu wengine au aina zingine za unyanyasaji wa kijinsia, ao tena kazi ya kulazimishwa au huduma ya kulazimisha, utumwa au hali za sawa na utumwa, kulazimishwa kufanya kazi au kuondolewa kwa viungo vya mwili;
>
> *Utumwa:* "Utumwa ni hali au mazingira ya mtu ambaye nguvu za haki ya kumilikiwa kwake zinatendwa juu yake kwa sehemu ao kwa jumla."

✔ Nina umri wa miaka 18 ao zaidi.

✔ Ninajiunga kama mtu binafsi na sio kama mwakilishi wa shirika.

✔ Niko tayari kujulisha jina langu la kwanza na la mwisho na adresse (anwani) ya kweli ya adresse email (barua pepe).

✔ Ninaelewa kuwa Jamii ya Walioponyoka (Walio Nusurika) ya Survivor Alliance haiwapi watu huduma za moja kwa moja kama makazi, matunzo, au msaada wa kisheria lakini inaweza kupana maelekezo.

**Maswali yanayohusu Kujiandikisha kama Mwanamemba**

Asante Kuona Unayo nia ya kujiunga na Jamii ya Walioponyoka (Walionusurika)! Kabla ya kujaza kurasa hii, tunataka ujue kwamba habari maalum na ya kibinafsi unayotueleza itachungwa kama siri. Isipokuwa utupe ruhusa ya kuishirikisha wengine.

Walakini, habari itaongezwa na kusambazwa bila majina kwa watu wengine kwa kutumia taarifa kama vile: "25% ya washauri wa Shirika ya Walioponyoka ni wanao kaa katika “fulani", ao "57% ya washauri hutoa hotuba kuu".

Jina lako kamili______________________(inahitajika)

Anwani yako ya Email (Barua pepe)_____________(Inahitajika)

Je! Ni yapi ya maneno yafuatayo ambayo unatumia kuelezea uliyo wahi kuyapitia? (Inahitajika)

(Toa majibu kwa yote uonayo ilikuhusu)

Utumwa
Bihashara ya binadamu
Kulazimishwa kazi
Kazi ya dhamana
Utumwa wa nyumbani
Uaskari wa watoto
Utumwa sababu ya deni
Ndoa iliyolazimishwa
Bihashara ya ngono kwa Watoto (CSEC)
Bihashara ya ngono
Kunyanyaswa kwa bihashara ya wafanyikazi
Nyingine: _________________________________

Kwa sasa hivi naendelea kutoa huduma ya kusema, mafunzo, au ushauri katika uwanja wa kupambana na utumwa / mambo ya bihashara ya unyanyasaji wa binadamu. (Inahitajika kueleza)

Ndio

Hapana
Hapana, lakini nataka

Je! Wewe unaishi katika mji gani? (Hiari)

Unaishi katika nchi gani? (Inahitajika)

Tafadhali jibu kila sharti la kujiandikisha kama mwanamemba na ambalo linakuhusu. (INAHITAJIKA)

Nina umri wa miaka 18.

Ninajiunga na Jumuiya ya Walionusurika kama mtu na sio kama mwakilishi wa shirika.

Nimesoma Makubaliano yanayo hitajika kwa kuwa Uwanamemba.

Ninakubali kuruhusu wafanyakazi wa Shirika la Walioponyoka (Walionusurika) -Survivor Alliance- waingilie uchunguzi kunihusu ikiwa wanashakia kuwa mimi sishikilie vizuri Makubaliano ya kuwa Mwanamemba. Ninaelewa kuwa naweza kupoteza haki yangu ya kuwa mwanamemba ikiwa ninavunja Makubaliano hii inayo hitajika kwa Wanamemba.

Ningependa kupokea mashauri ya bure kuhusu maelezo ya historia ya maisha yangu binafsi. Ndio
Hapana

Napenda kupokea bila malipo ushauri kuhusu historia ya elimu na kazi nilizo wahi kuzifanya (CV).
Ndio
Hapana

Tutakuwa tukilituma jarida la kila mwezi inay eleza habari ya mambo tulio yafanya, Katika Kundi la Survivor Alliance pamoja pia na a) habari kuhusu wapi kunahitajika Washauri kama hitaji liko na / au jinsi ya kupokea maendeleo ya kujielimisha na b) vifaa vya habari zinazo husu Makundi duniani inayo yanayo piganisha hali za utumwa.
Je! Ungependa kukuwa na pokea jarida hili? (Jibu linahitajika):

Ndio, tafadhali nitumieni jarida!
Hapana, sitaki kupokea jarida hili i

Tafadhali toa majina na anuani ya email (barua pepe)/barua za mtu/watu waliokuelekeza kwa Survivor Alliance (Tafadhali kumbuka kuwa, tutawasiliana na anuani ya barua pepe uliyotoa ili kujuwa Habari na kupata mahakikisho kukuhusu. Hata ikiwa kama haukuelekezwa na mtu yeyote, bado tutakuwa tu na nia ya kukaribia. Tunaomba maelezo haya ili yatusaidie kuhusiana na usalama wa jamii ya Survival Alliance) :

.............................................. .................................................

Tunataka kuwa na mazungumzo mafupi na ya kirafiki pamoja nawe kabla ya kukuongeza kama mwanachama. Tunahitaji mazungumuzo hayo ili tuweze kujifunza zaidi kukuhusu, kuhakikisha unajua tunachotoa, na pia ili kuweza kuambatanisha uso wa mtu na jina lake. Tafadhali tuambie saa za eneo lako na upendekeze tarehe na nyakati unaoweza kuwa huru kwa mazungumzo kwa dakika 30 kwa kupitia Zoom. *

................................................ .....

Tafadhali tuambie ni vikundi au mashirika gani mengine ambayo umeunganishwa nayo. Unaweza kuongeza viungo vyovyote vya mahojiano na utuambie kazi ambayo umesha wahi kuifanya kama Kiongozi/Munusurika.

................................................ ........

Maswali mengine yoyote unayo kwetu? ________________________________________